

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU, MH. PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB.), KATIKA SIKU YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI DUNIANI - DODOMA, 28 APRILI 2022**

- Mhe. Anthony Mtaka - Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;
- Mhe. Umy Nderiananga (Mb.) – Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu;
- Prof. Jamal A. Katundu – Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; na Makatibu Wakuu wote mliopo;
- Dkt. Fatma Mganga - Katibu Tawala, Mkoa wa Dodoma;
- Mhe. Jabir Shekimweri - Mkuu wa Wilaya, Dodoma Mjini;
- Mhe. Joseph Mhagama (Mb.) – Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria;
- Mhe. Najma Giga – Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Bunge;
- Wahe. Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria;
- Dkt. Adelhem Meru – Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri OSHA;
- Bi. Khadija Mwenda - Mtendaji Mkuu OSHA;
- Bi. Suzan Mkangwa – Kamishna wa Kazi (OWM – KVAU)
- Bw. Tumaini Nyamhokya – Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA);
- Bw. Kheri Mkunda – Katibu Mkuu, TUCTA
- Bi. Suzane Ndomba - Mkurugenzi Mtendaji, ATE;
- Bi Getrude Sima – Mwakilishi wa ILO;

- Wakuu wa Idara na Vitengo – Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu;
- Wakurugenzi kutoka Wakala wa Usalama na afya Mahali pa Kazi (OSHA);
- Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi mliopo;
- Ndugu Washiriki wa Maonesho;
- Wageni Waalikwa;
- Waajiri na Wafanyakazi wote;
- Mabibi na Mabwana.

### ***Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***

Kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujaalia sote kuwepo hapa leo, katika Maadhimisho ya Siku ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani, tukiwa wazima wa afya njema. Pia napenda kuwashukuru wote mliohudhuria katika maadhimisho haya kwani inaonesha ni jinsi gani mnavyounga mkono juhudi za kuboresha mazingira ya usalama na afya pahali pa kazi.

Hali kadhalika, napenda kuwashukuru waandaaji wa maadhimisho hayo ambayo yametukutanisha hapa leo na pia kwa kunikaribisha kuwa Mgeni Rasmi katika siku hii muhimu tunapoungana na wenzetu Duniani kote katika kuadhimisha siku hii.

Nawapongeza pia wajasiliamali wadogo ambao wamepata elimu ya usalama na afya mahali pa kazi katika Kanda mbalimbali kuanzia tarehe 24/4/2022 ikiwa ni sehemu ya kuelekea kilele cha maadhimisho haya, pamoja na wale mliopata mafunzo leo hapa katika viwanja hivi. Wito wangu kwenu ni kutumia elimu mliyopata kujikinga na vihatarishi ambavyo vinaweza kuhatarisha afya na usalama wenu mara mtakaporudi katika shughuli zenu za kuzalishaji mali.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Uongozi wa Mkoa wa Dodoma hususan Mkuu wa Mkoa wa Dodoma (Anthony John Mtaka) kwa kukubali kuwa mwenyeji wetu katika kuadhimisha siku hii, na ametupatia ushirikiano wa hali ya juu sana. Niwashukuru pia Viongozi wa Utatu (Serikali, TUCTA na ATE) ambao pia wameshiriki kikamilifu katika kuhakikisha kuwa siku hii ya leo inafanikiwa kama tunavyoona

hivi sasa. Niwapongeze pia wenzetu wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa kuwa wameendelea kushirikiana na Serikali katika masuala yote yanayohusu kazi na ajira.

Mwisho lakini sio kwa umuhimu nawapongeza wadau wetu wote mliokuja kufanya maonesho haya ya Usalama na Afya mahali pa kazi pamoja na Mei Mosi. Kwa hakika maonesho haya yemefana sana. Hivyo, nichukue fursa hii kuwashawishi wale ambao hawakuweze kufika kwa sababu mbalimbali, ili wafike mwakani na miaka ijayo waweze kuonesha juhudi zao za namna wanavyo imarisha usalama na afya kwa wafanyakazi wao. Maonesho haya hufanyika kila mwaka.

Ndugu wafanyakazi na waajiri, leo tumekusanyika hapa kuadhimisha siku ya usalama na afya mahali pa kazi Duniani. Hii ni siku ya Kimataifa ya kufanya kampeni ya kuboresha usalama na afya wa wafanyakazi. Lengo ni kuondoa hali zote hatarishi mahali pa kazi na hivyo kuifanya kazi iwe ya hadhi na heshima. Siku hii inaadhimishwa kwa namna mbalimbali katika Nchi zaidi ya 110 Duniani. Baadhi ya shughuli ambazo zinafanyika katika maadhimisho haya ni kama vile

maandamano, makongamano ya uhamasishaji, pamoja na upashanaji habari.

Tunapokuwa tunafanya maadhimisho ya siku hii, tunakuwa na malengo makuu yafuatayo: Kuongeza uelewa kuhusu ukubwa na madhara ya ajali na magonjwa yatokanayo na kazi miongoni mwa waajiri na wafanyakazi; Kuhamasisha namna ya kulinda usalama na afya za Wafanyakazi wakiwa kazini hasa kwa kuzingatia kanuni za kazi Kitaifa na Kimataifa; na Kuhamasisha Wadau mbalimbali kujenga uwezo na utaalamu wa kuweka mifumo, sera na mikakati inayolenga kulinda usalama na afya za wafanyakazi wakiwa kazini.

Waajiri na wamiliki wa sehemu za kazi katika Nchi nyingi duniani hasa zinazoendelea, Tanzania ikiwa mojawapo hudhani kuwa kuweka mazingira ya kazi salama ni gharama za ziada katika kufanya biashara. Hii yawezekana ni kwa kukosha ufahamu wa faida za kuboresha mazingira ya kazi na hasara zinazoweza kutokea hususan inapotokea ajali au ugonjwa katika sehemu ya kazi. Mtazamo huu unafanya tuendelee kuona matukio makubwa katika sehemu za kazi yanayosababisha Wafanyakazi kupata ulemavu wa kudumu,

kupata magonjwa yanayotokana na kazi na hata kusababisha kupoteza maisha.

Makaridio ya Shirika la Kazi Duniani na Shirika la Afya (ILO) na Afya (WHO) Duniani ya mwaka 2016 yalionesha kuwa takribani wafanyakazi milioni 1.9 wanafariki Duniani kote kutokana na ajali na magonjwa yatokanayo na kazi. Makadirio hayo yalizingatia vihatarishi 19 mahali pa kazi, ikiwa ni pamoja na kufanya kazi muda mrefu (long working hours), uchafuzi wa hewa mahali pa kazi, vihatarishi vinavyosababisha magonjwa ya pumu na saratani, vihatarishi vya egonomia, na kelele. Kihatarishi kikubwa kilikuwa ni kufanya kazi kwa muda mrefu, kilichohusishwa na takriban vifo 750,000, ikifuatiwa na uchafuzi wa hewa mahali pa kazi uliosababisha vifo 450,000.

Kwa upande wa Tanzania, katika kipindi cha miaka mitano (2016 - 2020) taarifa za ajali na magojwa 6,846 ziliwasilishwa katika Mfuko wa Fidua kwa Wafanyakazi (WCF) kwa ajili ya fidua. Na katika ajali na magonjwa hayo asilimia 26.4 zilitokea wakati wafanyakazi wakiwa safarini katika kutekeleza majukumu ya kikazi na asilimia 5.3 ya ajali hizo zilisababisha vifo. Kwa takwimu hizo inasikitisha kuona jinsi ambavyo kazi

zinaweza kusababisha ulemavu wa kudumu na hata vifo kwa wafanyakazi. Hali hii haipaswi kuachwa ikaendelea, ni lazima tuchukue hatua stahiki.

Ajali na magonjwa hayo yanayotokea sehemu za kazi, yanaongeza gharama za uzalishaji na utoaji wa huduma kwa Mwajiri na Taifa kwa ujumla. Gharama hizo ni kama matibabu, malipo ya fidia, uharibifu wa mali mbalimbali, kupotea kwa muda wa uzalishaji, gharama za kufundisha mfanyakazi mwingine iwapo aliyeumia hataweza tena kurudi kazini na kadhalika. Kwa mujibu wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), gharama hizo zinafikia kati ya asilimia 3 - 4 ya pato la Taifa (GNP) la Nchi husika.

Mwaka huu tunapoadhimisha siku hii kauli mbiu Duniani kote ni **“Kwa pamoja tushirikiane kujenga utamaduni bora wa usalama na afya mahali pa kazi (Act together to build a positive safety and health culture)”**.

Utamaduni huu unahitaji haki ya mazingira salama ya kufanyia kazi iheshimiwe katika ngazi zote. Ni utamaduni unaohitaji kuona Serikali, Waajiri na Wafanyakazi wanashiriki

kikamilifu katika kuweka mazingira salama ya kufanya kazi kupitia mfumo wa haki na wajibu ulioainishwa, ambapo kanuni ya kuzuia vihatarishi inapewa kipaumbele cha juu zaidi.

Kupitia majadiliano ya pamoja, Wadau wa Utatu (Serikali, Waajiri, na Wafanyakazi) watashiriki kikamilifu katika hatua zote za mchakato wa kufanya maamuzi ya kulinda usalama na afya za wafanyakazi. Majadiliano ya pamoja yatachangia kuboresha sera na mikakati ya usalama na afya mahali pa kazi na utekelezaji wake kwa haraka na ufanisi zaidi. Sera na mikakati hiyo itaweka haki na wajibu wa kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa msingi wa kuweka mazingira salama ya kazi ni kuzuia au kupunguza vihatarishi vinavyoweza kupelekea ajali au magonjwa yatokanayo na kazi.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na wananchi** kwa ujumla, ukiuliza wafanyakazi sababu ya ajali kutokea, wengi wao watajibu kuwa ajali ni matokeo ya mazingira mabaya ya kazi na ukiuliza waajiri wao watajibu kuwa ajali ni uzembe wa wafanyakazi. Kwa namna nyingine, hii inadhihirisha kuwa jamii yetu haijui kwa ufasaha visababishi vya ajali na magonjwa yanayotokea mahali pa kazi. Ukweli ni kwamba



kwa asilimia kubwa jambo ambalo linasababisha ajali kwa kiwango kikubwa ni makosa ya kibinadamu. Na makosa mengi ya kibinadamu yanatokana na kutokuwa na utamaduni wa kuzuia vihatarishi. Hivyo tunapoadhimisha siku hii ya leo, ni vema kuwahimiza wadau wote wawe na mjadala mpana wa namna ya kuimarisha utamaduni wa kuzuia vihatarishi miongoni mwa jamii yetu.

Moja ya mambo yatakayotuwezesha kuimarisha utamaduni wa kuzuia vihatarishi ni kuweka mifumo madhubuti ya usalama na afya mahali pa kazi inayolindwa na Sheria, kuimarisha ukaguzi, kutoa mafunzo na kuongeza utaalam kwa waajiri na wafanyakazi. Ili kufanikiwa katika hili, waajiri na wafanyakazi kwa pamoja ni lazima wachukulie kwamba afya na usalama mahali pa kazi ni sehemu ya mipango ya uzalishaji au utoaji wa huduma.

**Ndugu Wadau**, tangu mwishoni mwa mwaka 2019, Dunia ilipita katika wakati mgumu ambapo Mataifa yote yalikuumbwa na janga la ugonjwa hatari wa UVIKO-19. Janga hili liliweka wafanyakazi na watu wote Duniani kwenye hali hatarishi ya kuambukizwa Virusi vya Korona katika mazingira ya kazi.

Baadhi ya wafanyikazi ambao walikuwa kwenye hatari zaidi ya kuambukizwa virusi hivyo ni wafanyakazi wa huduma za dharura, watoa huduma za afya na wafanyakazi wanaotoa huduma za kijamii. Janga la UVIKO-19 hasa wimbi la kwanza na la pili lilisababisha Serikali, Waajiri, Wafanyakazi na jamii kwa ujumla kukabiliwa na changamoto kwenye ulimwengu wa kazi ambazo hazijawahi kutokea Duniani katika siku za karibuni. Hali hiyo ilipelekea kuwepo na majadiliano ya Utatu ya jinsi ya kuweka mikakati bora ya kukabiliana na janga hilo.

Janga la UVIKO-19 limesababisha athari kubwa katika sehemu za kazi na limegusa karibu kila sehemu ya kazi. Licha ya kuwa janga hili linaleta hatari ya kuambukiza virusi vya Korona katika sehemu za kazi, lakini pia limekuwa ni kihatarishi kipya cha usalama na afya kazini (OSH Risk). Janga hili lilileta mabadiliko ya aina mpya ya ufanyaji kazi, mfano kufanyakazi kutokea nyumbani, hali ambayo ilisababisha vihatarishi vya kisaikolojia.

Pamoja na kuwa maambukizi ya Virusi vya Korona yamepungua, Janga hili bado lipo. Hivyo, nichukue fursa hii kuwataka Waajiri kwa kujadiliana na Wafanyakazi, wachukue

hatua zaidi za kuzuia kuibuka kwa wimbi jingine la maambukizi ya virusi hivyo. Hatua hizo zinalenga kuongeza tahadhari ili kuwakinga Wafanyakazi wasipate maambukizi mapya katika sehemu za kazi. Waajiri wanatakiwa kuchukua tahadhali kubwa kama zilivyoelekezwa na wataalamu wetu wa afya. Pia wafanyakazi wanapaswa kuzingatia usalama wao na watu wanaowazunguka sehemu za kazi bila kujali kama wana dalili za UVIKO-19 au la. Baadhi ya hatua hizo ni kama vile kupata chanjo ya UVIKO-19; kujitenga mara dalili za ugonjwa zinapojitokeza; kuzingatia umbali kati ya mfanyakazi mmoja na mwingine; na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima wakati wa mapumziko kazini au nje ya mahali pa kazi. Tahadhari nyingine ni kama vile kuepuka kuchangia vifaa na zana za kazi; kusafisha mara kwa mara zana na vifaa vyote vinavyotumiwa na watu wengi; kunawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka n.k.

**Ndugu wadau na ndugu wananchi,** sambamba na hilo Virusi Vya UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukiza bado ni masuala ya usalama na afya mahali pa kazi yanayopaswa kupewa kipaumbele miongoni mwa jamii ya Watanzania. Hii ni kwa sababu nguvu kazi inayotegemewa na Nchi ndiyo

iliyoko kwenye hatari ya kuambukizwa VVU. Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO), inaonyesha kuwa tangu kuanza kwa janga hili katika miaka ya 80, takriban watu milioni 79.3 wameambukizwa virusi vya UKIMWI na kwa wastani wa watu milioni 36.3 wamekufa kwa VVU. Takwimu zinaonesha kuwa jumla ya watu milioni 37.7 Ulimwenguni walikuwa wakiishi na VVU mwishoni mwa 2020. Inakadiriwa kuwa asilimia 0.7 ya watu wazima wenye umri wa miaka 15-49 Duniani kote wanaishi na VVU. Hata hivyo ukubwa wa janga hili unatofautiana kwa kiasi kikubwa kati ya Nchi na Nchi. Bara la Afrika hususan kusini mwa Jangwa la Sahara, madhara ni makubwa zaidi kiasi kwamba, karibia kila mtu 1 kati ya watu wazima 25 (3.6%) anaishi na VVU na idadi hiyo ni zaidi ya theluthi mbili ya watu wote wanaoishi na VVU Duniani.

Kwenye ripoti ya Tume za kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na wadau wengine iliyotolewa mwaka 2016-17 ilionesha kuwa, katika Tanzania maambukizi ya VVU ni asilimia 4.9 na maambukizi mapya ya kila mwaka ni wastani wa asilimia 0.25.

**Ndugu wadau, ndugu wananchi**, takwimu hizi bado sio za kupendeza hasa katika eneo la kusini mwa jangwa la Sahara. Kama vile haitoshi jambo baya zaidi ni pale ambapo asilimia 80 ya watu wanaoathirika na ugonjwa huo ni wale walio kati ya umri wa miaka 20 hadi 44 ambao ndio wanaotegemewa kufanya kazi ili kuinua uchumi wa Nchi. Wafanyakazi wanapoathiriwa na huu ugonjwa hawawezi kuzalisha mali kwa ufasaha, hali inayolazimu waajiri kulazimika kuajiri na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wapya. Mchakato huu wa kuajiri na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wapya ni kuongeza gharama za uzalishaji. Hivyo, ni lazima sote tushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

**Ndugu Wananchi**, Wafanyakazi wa Tanzania wanakabiliwa na tishio la magonjwa sugu yasiyoambukiza (Non-Communicable Diseases), kama vile ugonjwa wa moyo, saratani na kisukari. Katika siku za nyuma magonjwa yasiyoambukiza yalidhaniwa kuwa ni tatizo la Nchi zenye kipato kikubwa. Hata hivyo, takwimu zinaonyesha kuwa magonjwa haya yana athari kubwa kwa Nchi zinazoendelea pia. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani, (WHO) ni kwamba

takriban asilimia 77 ya vifo vinavyosababishwa na magonjwa yasiyoambukiza hutokea kwenye Nchi zenye kipato cha chini na kipato cha kati.

Halikadhalika, magonjwa yasiyo ya kuambukiza nayo ni tatizo linaloongezeka Nchini Tanzania. Kundi linaloathiriwa sana ni wafanyakazi. Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma na Binafsi pamoja na Wafanyakazi kwa ujumla wana uwezekano mkubwa wa kupata magonjwa yasiyoambukiza kuliko watu wa kawaida. Hali hii kwa kiasi fulani inasababishwa na aina ya kazi ambazo hazihusishi kushughulisha mwili pamoja na ulaji wa vyakula usiozingatia mahitaji muhimu ya mwili. Aidha wafanyakazi katika baadhi ya Sekta za kiuchumi mfano katika sekta za ujenzi, uchimbaji wa madini, kilimo nk, wanaathirika na magonjwa sugu yasioambukiza kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya kemikali na vihatarishi vingine katika sehemu za kazi.

Katika suala hili ni vizuri pia tukajenga utamaduni wa kuzuia magonjwa haya kwa kuwa matibabu yake ni ya muda mrefu na yanagharimu fedha nyingi. Katika Nchi yetu tumetayarisha Mkakati wa Taifa wa Magonjwa yasiyoambukiza na tunafanya

juhuri za kuimarisha huduma za matibabu hapa nchini. Lakini pia ni vizuri kuhimiza mazoezi na michezo miongoni mwa wafanyakazi hasa makundi yaliyo kwenye hatari kubwa, kuhimiza ulaji wa vyakula bora, matumizi sahihi ya kemikali na kuzuia vihatarishi kwa wafanyakazi katika baadhi ya sekta za kiuchumi.

**Ndugu wadau, ndugu wananchi,** yapo pia magonjwa mengine mengi yanayowapata wafanyakazi katika sekta zote za uzalishaji wakati wakiwa kazini. Kutambua ugonjwa unaotokana na kazi inapaswa kufanya uchunguzi wa kina kama kuna uhusiano kati ya ugonjwa husika na vihatarishi katika sehemu ya kazi. Uhusiano huo unathibitishwa kwa kuchukua historia kamili ya mazingira ya kazi na kuthibitisha bila mashaka kuwa kazi aliyokuwa anafanya mfanyakazi husika ina uwezekano wa kusababisha ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa wataalam wetu, magonjwa yatokanayo na kazi yanakuwa sio rahisi kuyatambua mapema kwa kuwa yanachukua muda mrefu sana (kati ya miaka 15 hadi 20) tangu mfanyakazi anapopata ugonjwa husika hadi ugonjwa huo kujitokeza. Na bahati mbaya zaidi ni kuwa mara baada ya

kujitokeza, inakua sio rahisi magonjwa hayo kutibiwa. Ni jambo la muhimu kukumbuka pia kwamba hali halisi ya magonjwa yatokanayo na kazi inabadilika sana hasa ukizingatia kuwa teknolojia, utandawazi na mabadiliko katika jamii yana uhusiano wa karibu na magonjwa hayo. Magonjwa yaliyozoeleka miongoni mwa wafanyakazi ni matatizo ya mfumo wa hewa, kupoteza uwezo wa kusikia na madhara yanayosababishwa na kemikali mbalimbali. Katika siku za karibuni msongo wa mawazo pamoja na matatizo ya misuri na mifupa (musculoskeletal disorders) mfano maumivu ya mgongo na shingo yatokanayo na kazi yameongezeka sana.

Serikali pia inathamini juhudi za Waajiri katika Sekta za Umma na Binafsi kwa kushirikiana na Wafanyakazi wanaojituma katika kuboresha mazingira ya kazi wao wenyewe bila kusukumwa. Hivyo kupitia Wakala wake wa Usalama na Afya mahali pa Kazi (OSHA), Serikali imeanzisha tuzo maalumu kwa Waajiri watakao kuwa wanaonyesha juhudi katika kuboresha mazingira ya kazi kwa kuweka mfumo ya afya na usalama kazini iliyo imara. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waajiri waliofanikiwa kupata tuzo mwaka huu. Lakini pia nichukue fursa hii kuwataka Waajiri wajitokeze kwa



wingi kushiriki kwenye tuzo za usalama na afya mahali pa kazi na maonesho katika miaka ijayo.

Mwisho ningependa kuisisitiza kuwa, inawathamini wafanyakazi na iko makini sana na usalama na afya mahali pa kazi. Hivyo Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wote ili kupunguza au hata ikiwezekana kuondoa kabisa vifo, ajali, magonjwa na madhara yatokanayo na kazi. Lengo ni kuhakikisha kuwa, mazingira ya kazi ni salama na hivyo kuongeza tija katika uzalishaji.

Baada ya kusema hayo, kwa mara nyingine napenda kuwashukuru wote mlioshiriki kikamilifu katika maadhimisho haya na napenda kisisitiza tena **“Wafanyakazi, Waajiri na wananchi wote kwa ujumla tafadhali tujiunge pamoja katika kufanya majadiliano ya namna bora ya kujenga utamaduni wa kuzuia ajali na magonjwa mahali pa kazi”**.

***“Afya yako ndio mtaji wako”***

Asante kwa kunisikiliza.